WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU MAMIRE

E-mail: mamiretc@gmail.com
ebsite:www.mamiretc.ac.tz

S.L.P. 561
Babati
Manyara

**Kumb.Na.MMR/TC/UTA/06/0053** **30 Mei 2025**

Ndg/Bi: ____________________________________

S.L.P: __________________________

__________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU MWAKA 2025/2026**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu kozi (Programu) Stashahada ya Ualimu, Elimu ya Msingi kwa mchepuo wa **Sayansi na Hisabati** katika Chuo cha Ualimu Mamire.

Chuo cha Ualimu Mamire kipo kata ya Mamire, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara, umbali wa Kilometa 16 Kaskazini Mashariki ya mji wa Babati. Wanachuo wanaojiunga na chuo hiki huchaguliwa kwa kuzingatia vigezo rasmi vya ufaulu katika mtihani wa kidato VI pamoja na ufaulu katika kozi ya Astashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi, vilivyowekwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuzingatia ufaulu wa mitihani ya Taifa kwa ngazi husika. Chuo kinakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu katika chuo hiki; hongera sana.

## 2.0 TAREHE YA KUANZA MAFUNZO

Mafunzo ya Ualimu kwa wanachuo wa mwaka wa kwanza ngazi ya **Stashahada ya Elimu ya Msingi** yataanza tarehe **18 Agosti 2025, unapashwa kuripoti chuoni kwa tarehe tajwa.**

Ripoti chuoni siku hiyo kwa ajili ya usajili na kuanza rasmi mafunzo. **Tafadhali fika chuoni mapema muda wa masaa ya ofisi/kazi sio usiku.**

Mara ufikapo chuoni fuata taratibu za kiusajili zilizowekwa ukiwa na **vyeti halisi** (sio nakala) na viambatanisho vyote. **Karibu chuo cha Ualimu Mamire.**

## 3.0 HUDUMA MUHIMU:

Huduma muhimu zifuatazo zinapatikana chuoni Mamire.

**3.1 CHAKULA**: Wanachuo wote hupatiwa chakula chuoni katika bwalo la chakula. Chuo hakina uwezo wa kutoa huduma ya chakula maalum (special diet) kwa wanachuo wenye uhitaji huo.

**3.2 AFYA**: Chuo kipo karibu na kituo cha afya Mamire ambapo mwanachuo anaweza kupata huduma ya matibabu kwa gharama nafuu. Matibabu zaidi hupatikana katika hospitali ya mji wa Babati au Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Manyara kwa mwanachuo kujigharamia mwenyewe. Wanachuo wote wanapaswa kujiunga na huduma ya Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) kwa kulipia **Tsh. 50,400.00 kwa mwaka**. Iwapo unayo kadi ya Bima ya afya,ambayo ni hai unashauriwa kuja nayo**. Tafadhali zingatia maelekezo ili kuepusha usumbufu utakaoweza kujitokeza mara upatapo changamoto ya kiafya.**

Taratibu za kujiunga na Bima ya afya baada ya kuchangia zitaratibiwa chuoni kwa kushirikiana na Uongozi wa Bima ya Afya ya Mkoa).

**3.3 HUDUMA ZA KIFEDHA**: Huduma za benki zinapatikana mjini Babati katika matawi ya benki ya NMB, NBC, CRDB na Benki ya Posta, pamoja na mawakala wao waliopo Mamire. Uongozi wa chuo unashauri wanachuo kuhifadhi fedha zao benki au kwa kutumia huduma za fedha zitolewazo na makampuni ya simu kama vile M-Pesa, Tigo-pesa/Mix by Yas , Airtel money, n.k.

**3.4 USAFIRI**: Usafiri wa kufika Mamire kutoka mjini Babati kwa kutumia magari ya abiria( public transport) unapatikana kwa urahisi kuanzia saa 1.00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kwa gharama ya shilingi 1,500/= - 2,000/=, kwa kila abiria. Usafiri wa Bajaji ni wa uhakika zaidi kutoka Babati mjini, kituo cha kona ya Mrara hadi Chuoni Mamire.

**3.5 MALAZI**: Malazi yanapatikana bure katika mabweni ya chuo. Unatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi binafsi bwenini:-

i. Shuka mbili – “Blue” bahari.

ii. Mto na foronya mbili – “Blue” bahari.

iii. Blanketi rangi ya bluu/ yenye maua ya bluu.

iv. Chandarua cha mviringo/mraba ft 4x6 au zaidi.

v. Ndoo (2) za maji zenye ujazo wa lita kumi (10) kila moja kwa matumizi binafsi.

vi. Sanduku imara lenye kufuli kwa utunzaji salama wa vifaa vyako.

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikom be na kijiko) **visiwe vya plastiki.**

viii. Taulo za kike za kutosha.

ix. “Toilet papers” (5) au zaidi kwani vyoo ni vya maji.

x. Taulo ya kujifutia

xi. Nguo za ndani za kutosha.

xii. Vibanio 12 au zaidi vya kubania nguo wakati wa kuanika.

xiii. Nguo binafsi zenye staha na zinazoendana na maadili ya kazi ya ualimu utakayosomea.

xiv. Sabuni ya kufulia (sabuni ya unga/kipande), mafuta ya kujipaka, mswaki na dawa ya meno.

xv. **Kwa waumini wa kiislamu**: wanaume waje na kanzu nyeupe na wanawake waje na baibui nyeusi kwa ajili ya kwenda msikitini siku za ibada.

xvi. Begi la mgongoni kwa ajili ya kubebea madaftari na vitabu.

xvii. Tochi au Taa ya kuchaji kwa mwanga wa jua (solar).

xviii. Fedha za matumizi binafsi (pocket money).

**Kumbuka: Vifaa vyote vilivyoagizwa vitakaguliwa wakati wa kuripoti**).

## 4.0 VYETI NA VITAMBULISHO:

**4.1** Wanaojiunga na mafunzo ya **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi** wanatakiwa kuleta vyeti/hati zifuatazo: -

i. Cheti halisi cha kidato cha nne (IV) kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

ii. Cheti halisi cha kidato cha sita kwa waliohitimu ngazi hiyo ya Elimu au result slip kwa waliohitimu mwaka 2025 ikiwa vyeti halisi havijatoka.

iii. Cheti halisi cha kuhitimu mafunzo ya Ualimu ngazi ya Astashahada ya Elimu ya Msingi (GATCE) kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa au Result slip kwa waliohitimu mwezi Mei 2025.

iv. School leaving certificate ya kidato cha nne, sita na ualimu

v. Cheti cha kuzaliwa;

vi. Barua ya mwajiri kukuruhusu kuja mafunzoni kwa waajiriwa;

vii. Medical Examination form iliyojazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali, (**fomu imeambatanishwa**). Hakikisha unafanyiwa vipimo vya afya vilivyoagizwa.

viii. Vyeti vya mafunzo mengine uliyopitia;

ix. Vivuli (photocopies) vya vyeti halisi vyote vya kitaaluma vilivyotajwa hapo juu kwa ajili ya matumizi ya kiofisi.

## 5.0 GHARAMA ZA UENDESHAJI

Kila mwanachuo anatakiwa kuchangia gharama za uendeshaji kama ifuatavyo:-

**5.1 Ada:** Ada ya mafunzo ni **TSh.450,000/=** kwa mwaka.

Ada hii inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili yaani **TSh.225,000/=** kwa muhula. Malipo ya ada yafanyike mwanzoni mwa Muhula.

Malipo ya ada yafanyike kupitia mfumo wa malipo ya fedha za serikali **Government e Payment Gateway** (GePG). Mwanachuo anatakiwa kuweka fedha zake kwenye mifumo ya fedha ya kielektroniki ili atakapofika Chuoni apatiwe namba ya utambulisho wa malipo (**Control number**) kwa ajili kufanya malipo.

**Kumbuka: Malipo ya ada yasifanyike kwenye akaunti ya michango**.

**5.2 Michango**: Mwanachuo atapaswa kukamilisha michango ifuatayo ili aweze kusajiliwa.

i. Kitambulisho na Usajili: TSh. 20,000/= kwa mwaka wa kwanza tu;

ii. Serikali ya wanachuo TSh. 5,000/= kwa mwaka;

iii. Godoro Tsh 10,000/= kwa mwaka;

iv. Ukarabati TSh. 25,000/= kwa mwaka;

v. Usafi na mazingira TSh. 20,000/= kwa mwaka;

vi. Ulinzi Tsh. 30,000/= kwa mwaka

vii. Elimu ya Michezo TSh. 30,000/= kwa mwaka;

viii. Huduma ya kwanza TSh. 10,000/= kwa mwaka;

ix. Mahafali 10,000/= kwa mwaka

Michango yote ilipwe kupitia akaunti namba **40710011350** yenye Jina la **Mamire Teachers College Reccurent A/C iliyopo benki ya NMB.**

Majina kamili ya mwanachuo (**kwa mujibu wa vyeti vyake vya kitaaluma**) yaandikwe katika fomu ya malipo (Pay-in- Slip).

**Kumbuka: Michango yote ilipwe mwanzoni mwa mwaka.**


## 6.0 SARE ZA CHUO

Wanachuo wote lazima wavae sare rasmi ya chuo wakati wa masomo, shughuli rasmi na wakati wa matembezi nje ya chuo. Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na sare kama ifuatavyo:


### 6.1 Wanaume:

i. Suruali mbili (2) rangi nyeusi (plain) – kitambaa imara kisichopauka haraka (kisiwe kitambaa cha kuteleza) (upana wa chini (mzunguko) **usipungue sm.16.**
ii. Koti jeusi - kitambaa imara kisichopauka haraka kinachofanana na suruali (kisiwe kitambaa cha kuteleza) au sweta jeusi la kufumwa (V-shape) shingoni.
iii. Mashati mawili mikono mirefu – rangi nyeupe, yenye vishikizo/vifungo vilivyoshonewa.
iv. Tai ndefu nyeusi;
v. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba; vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi nyeusi (**jozi 2**);
vii. Mkanda wa suruali mweusi usio na urembo.
viii. T-Shirt yenye nembo ya Chuo kwa TSh.20,000/= itapatikana chuoni.

**Zingatia:** Mashono ya suruali na koti yazingatie picha Na.1 na 2 kama inavyoonekana hapo chini. **Sare chakavu au mitumba hazikubaliki**.



***Picha 1***



***Picha 2***


**Kumbuka:** Sare ambazo hazitakidhi viwango vya ubora hazitakubalika.

### 6.2 Wanawake


i. Sketi mbili (2) nyeusi - kitambaa imara kisichopauka haraka (isiwe kitambaa cha kuteleza). Sketi iwe ya heshima, isiyobana na iwe ndefu hadi chini.
ii. Koti jeusi - kitambaa imara kisichopauka haraka inayofanana na sketi (isiwe kitambaa cha kuteleza) au Sweta jeusi la kufumwa kwa uzi (V-shape) shingoni.

iii. Mashati mawili (2) mikono mirefu – rangi nyeupe, yenye vishikizo/vifungo vilivyoshonewa.
iv. Tai ndefu rangi nyeusi;
v. Viatu vyeusi (jozi 2) vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi nyeupe, fupi (jozi 2)
vii. Ushungi mweupe usiokuwa na urembo kwa wasichana wa kiislamu watakaopenda kuvaa;
viii. T-Shirt yenye nembo ya Chuo kwa TSh.20,000/= itapatikana chuoni.

**Zingati**a :Mashono ya sketi na koti yazingatie mchoro **namba 3** na **namba 4** hapo chini



***Picha 3***



***Picha 4***

**Kumbuka:** Sare ambazo hazitakidhi viwango vya ubora hazitakubalika.

**7.0 VIFAA VYA TAALUMA:**

i. Daftari 10 quire 3, Kalamu za kutosha, Rula na faili (spring file) (10);
ii. Mathematical instruments' seti moja (1);
iii. Scientific Calculator;
iv. Rimu ya karatasi (01) kwa matumizi ya kitaaluma kwa mwaka.
v. Kalamu za rangi mbalimbali kwa ajili ya kuchorea vielelezo vya kufundishia;
vi. Kamusi ya kiingereza (English-English Dictionary)
vii. Vitabu viwili (02) (darasa la 3-6 )vya masomo ya kufundishia kwa mujibu wa tahasusi unayosomea na lugha ya kufundishia.
viii. Simu janja, Komputa mpakato, kishikwambi kwa wenye uwezo.

**8.0 VIFAA VINGINEVYO**

i. Uje na jembe (Lenye Mpini), Fyekeo, reki na soft broom kwa ajili ya usafi wa mazingira.

**9.0 NGUO ZA MICHEZO:**

i. Tracksuit (mpya)– “dark blue’” yenye mstari mweupe pembeni;
ii. T-Shirt na Bukta- bluu bahari (mpya) (zisizo na maandishi au picha) yoyote;
iii. Viatu vya michezo (raba) za kufunga kwa kamba.

**10.0 PICHA:**

Leta picha nne (4) passport size “Light blue background” kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

**11.0 KANUNI NA SHERIA ZA CHUO:**

Chuo cha Ualimu Mamire kama ilivyo vyuo vingine vya Ualimu, huendeshwa kwa kufuata sheria mbalimbali za nchi, kanuni, taratibu na sheria za chuo. (**Sheria na kanuni zimeambatishwa)** Soma na kuzielewa kabla ya kuripoti chuoni. Ufikapo chuoni utapewa maelekezo na ufafanuzi zaidi utakaoambatana na ujazaji wa fomu ya kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za chuo.

**12.0 MWISHO:**

Kumbuka kuwa siku zote mwalimu anapaswa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa mazuri na wanafunzi wake pamoja na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo kila mwanachuo anapaswa kuzifahamu, kuzingatia na kuzifuata ipasavyo sheria za nchi, kanuni na taratibu mbalimbali za chuo ili kuweza kutimiza malengo yaliyowekwa na chuo pamoja na wizara ya Elimu, sayansi na Teknolojia kwa ujumla. Hivyo basi, kila mwanachuo anatarajiwa kuwa na bidii katika kutekeleza majukumu mbalimbali atayoelekezwa ili kutimiza ndoto zake za kuwa mwalimu bora.

Kwa mawasiliano zaidi tafadhali piga simu namba zifuatazo:

**0754 45 11 00- Mkuu wa chuo, 0784189898-mwadili, 0786808016-ofisi ya Usajili**

Karibu sana Chuo cha Ualimu Mamire.

Jesca N. Moiro
**Mkuu wa Chuo**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**PART A:**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

From: The Principal,
Mamire Teachers' college,
P.O.Box. 561,
**BABATI - MANYARA**

To: The Medical Officer

____________________________________

____________________________________

REF: Mr/Mrs/Miss:__________________________________________________(Name in Full)

Please examine the above named as to *his/her physical and mental fitness for a full time teachers training course. The examination should include the following categories (I & II), each category or sub category of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (category II[b]) will also render a female candidate ineligible for the course.

**I**. (a) Eye sight (b) Hearing (c) Speech (d) Limbs (e) Venereal disease (f) Leprosy (g) Peptic ulcers (h) Epilepsy (i) Tuberculosis

**II.** (a) Neuroses (b) Pregnancy (c) Mental and Physical Fitness (d) Other Serious Diseases i.e. TB/HIV.

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by a Government Medical Officer)**

I have examined the above named and consider that *he /she is physically *fit/unfit for a full-time teachers' training course.

**I.** (a) Eye sight…………………… ……………………………………………………………….

(b) Hearing………………………………………………………………………………………

(c) Speech…………… ……………………………………………………………………………….

(d) Limbs……………….....................................................................................................

(e) Venereal disease……………… …………………………………………………………………

(f) Leprosy…………………………………………………………………………………………

(h) Peptic ulcers…………………… ….. …………………………………………………………...

(i) Tuberculosis………………………………………………………………………………

**II**. (a) Neuroses ……………………… ………………………………………………………..

(b) Pregnancy………………………………………………………………………………….

(c) Mental and Physical Fitness………………………………………………………………..

(d) Other Serious Diseases i.e. HIV…………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………………..

Name……………………………………..… Designation……………………………….
Date…………………………….................. Station…………………………………….

Signature ………………………...................... Official stamp:

***Delete whichever inapplicable**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU MAMIRE**

E-mail:mamiretc@gmail.com
Website:www.mamiretc.ac.tz

S.L.P 561,
Babati,
Manyara.

## KANUNI, SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

Chuo cha Ualimu Mamire ni chuo cha serikali na kinaongozwa sheria za nchi na sheria na kanuni zilizoainishwa katika mwongozo wa uendeshaji wa vyuo vya ualimu Tanzania.
Ili kumpa mwanachuo madaraka kamili juu ya tabia yake, chuo kina kanuni na sheria zifuatazo:

### MAADILI:

### A. Mavazi

i. Kila mwanachuo anapaswa kuvaa sare wakati wote na mahali popote akiwa chuoni, isipokuwa wakati wa kazi za nje baada ya masomo.
ii. Mwanachuo lazima avae sare ya Chuo wakati wote anapokuwa nje ya Chuo kwa shughuli zote za Chuo au zake binafsi.
iii. Mwanachuo lazima avae mavazi ya heshima awapo mafunzoni hapa chuoni.
iv. Vaa mavazi ya heshima uwe na haiba nzuri ya kiualimu (mavazi ni yale yaliyobainishwa katika mwongozo wa mavazi ya watumishi wa umma.
v. Mavazi ya heshima yavaliwe kulingana na shughuli husika. Mfano, michezo, shughuli mbalimbali nje ya darasa.
vi. Mwanachuo haruhusiwi kuingia bwaloni, darasani na maeneo ya utawala akiwa na mavazi yafuatayo: bukta, kandambili,"night dress," kofia, kanga, shuka n.k.

### B. LUGHA

i. Mwanachuo anapaswa kutumia lugha rasmi/fasaha katika mawasiliano (kiingereza au Kiswahili)
ii. Ni marufuku kutumia lugha za matusi au kashfa katika mawasiliano yoyote .

### C. HESHIMA NA UTII KWA TARATIBU ZA CHUO

i. Kila mwanachuo ajiheshimu mwenyewe kwa kuweka mwili wake na mavazi yake katika hali ya usafi na heshima.
ii. Kila mwanachuo awaheshimu wenzake, viongozi, wageni, walezi wote na watu wengine anaokutana nao hapa Chuoni na nje ya chuo. Siku zote kuwa kielelezo chema cha mtu aliyeelimika.
iii. Wanachuo wote wanapaswa kuishi kwa uhusiano wa kaka na dada na pia kuishi na walezi kama mama na baba na si vinginevyo. (**Ni kosa kwa wanachuo kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtu yeyote katika mazingira ya mafunzo.**
iv. Kila mwanachuo apaswa kuwa mfano bora kwa kauli, nidhamu na matendo mema.
v. Kila mwanachuo anapaswa kuwa na kiasi katika starehe. Ulevi wa aina yoyote ni mwiko.
vi. Kila mwanachuo anapaswa kuwa mkweli na mwaminifu kila wakati.
vii. Wanachuo wanapaswa kutunza na kulinda mali ya umma, mali yake na mali za wenzake. Uharibifu wa aina yeyote hautavumiliwa.
viii. Chakula kitaliwa bwaloni/kantini. Hairuhusiwi kujipikia mahali popote katika eneo la chuo. Ni marufuku kuingiza vyakula kutoka nje ya chuo.

ix. Ni marufuku kufanya mikutano ya aina yoyote pasipo kupata kibali rasmi kutoka kwa mwadili.
x. Masuala yote yanayohusu wanachuo yaripotiwe kwanza ofisi ya masuala ya wanachuo (uadili).

**D. MIPAKA:**

i. Ni marufuku kwa wanachuo wa kike (wanawake) kwenda bweni la wanachuo wa kiume (wanaume) au wanaume kwenda bweni la wanachuo wa kike.
**ii.** Ni kosa kwa wanachuo kujiingiza katika tabia ya uasherati au uzinzi na mtu yeyote.
**iii.** Ni marufuku kwa wanachuo kutembelea nyumba za watumishi isipokuwa kwa kibali maalum kutoka ofisi ya uadili au mkufunzi wa zamu.

**E. WAJIBU:**

i. Wanachuo wanapaswa kuwahi wakati wote anapohitajika, kwa kengele au ishara nyingine.
ii. Wanachuo wanapaswa kutimiza wajibu atakaopangiwa ndani na nje ya darasa.

**F. RATIBA:**

**i.** Wanachuo wanapaswa kufahamu, kuheshimu na kuifuata ratiba ya chuo katika utekelezaji wa majukumu yao.

**G. RUHUSA:**

i. Ruhusa ndogo (muda mfupi) kwenda maeneo ya karibu na Chuo zitatolewa na mwadili au mkufunzi wa zamu.
ii. Ruhusa za kwenda maeneo ya mbali na chuo (mfano Babati n.k.), kuwa nje ya chuo usiku au kulala nje ya Chuo, lazima zipate kibali cha Mkuu wa Chuo.

**H. MATUMIZI YA SIMU:**

**i.** Hairuhusiwi kutumia simu wakati wa vipindi au katika kusanyiko rasmi isipokuwa kwa ruhusa maalum (**unapaswa kuzima simu au kuweka kwenye hali ya mtetemo).**

**A. WAGENI:**

i. Wanachuo hawataruhusiwa kutembelewa na wageni wakati wa vipindi au shughuli rasmi.
ii. Wageni wa wanachuo wataruhusiwa kwa muda mfupi hasa siku zisizo za kazi (Jumamaosi na Jumapili) mchana.
iii. Wageni hawaruhusiwi kuingia madarasani, bwenini au bwaloni, sehemu ya mapokezi itakuwa getini.

I. **MATENGENEZO**:

i. Ni marufuku kwa mwanachuo yeyote kufanya matengenezo katika mifumo yoyote au vifaa vyovyote vya chuo pasipo kibali kutoka kwa mlezi. Toa taarifa kwa walezi,uharibifu/changamoto inapojitokeza.
ii. Ni marufuku kutumia umeme kwa matumizi mengine zaidi ya kuchajisha simu au "computer."

**Kumbuka**:
Yafuatayo ni makosa yanayoweza kumfanya mwanachuo aondolewe katika mafunzo bila maonyo ya awali:
i. Wizi ii. Utoro iii. Uzinzi iv. Kuwa mjamzito v. kutoa mimba vi. Kupiga/kupigana na mtu yeyote vii.Kugoma au kushawishi wanachuo wengine kugoma viii. Ulevi ix. Makosa ya jinai kwa kuvunja sheria za nchi x. Kuharibu mali/vifaa kwa makusudi.